

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI

24 JUNI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI TAREHE 24 JUNI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

663. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha wastani wa uwezo wa Halmashauri zetu kujitegemea unaongezeka na kuweza kukopa.

664. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Songambe - Kyerwa.

665. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi katika maeneo ya Vijijini.

WIZARA YA AFYA:

666. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza vifo vya Mama na Mtoto katika Mkoa wa Katavi ambapo kuna ongezeko kubwa kwa sasa.

WIZARA YA UJENZI:

667. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara ya Tengeru kwenda Mererani utaanza.

668. MHESHIMIWA DKT. ALFRED JAMES KIMEA (KOROGWE MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini TANROADS watamaliza zoezi la kuweka Taa Barabara ya Dar es Salaam - Arusha katika Mji wa Korogwe.

WIZARA YA FEDHA:

669. MHESHIMIWA MOHAMED SAID ISSA (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Akaunti ya Pamoja ya Fedha ya Zanzibar na Tanzania Bara itafunguliwa.

670. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupambana na uraibu wa Mchezo wa Kamari unaoongezeka kwa kasi kwa Vijana.

WIZARA YA KILIMO:

671. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kwa nini Serikali isiruhusu Mbolea kuwekwa kwenye vifungashio kuanzia kilo moja na zaidi ili kukidhi mahitaji ya Wakulima.

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

672. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, kuna mkakati gani wa kutengeneza vipaji vya Wachezaji wa Mpira wa Miguu nchini.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

673. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, lini Serikali itawakabidhi Wananchi wa Kijiji cha Nengungu eneo lao linalong'ang'aniwa na Chuo cha Jeshi Monduli.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

674. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali haioni haja ya kutenganisha upimaji wa Viwanja kila Mwananchi aweze kujenga uzio wa kujitegemea ili kuwe na *"no man's land"*.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

675. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kuna mpango gani kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa ambao unakwenda taratibu na ni muhimu kwa Watanzania.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

676. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo Kikuu katika eneo la Sasanda Mkoani Songwe.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
24 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**